**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**(TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**
**SHULE YA SEKONDARI NATTA**

**S.L.P 192 Mugumu-Serengeti.**
**Simu :0762177350, 0715103790 au 0753741530**
**E-mail: nattasec2004@gmail.com**

**Kumb. Na. NATT/F.I/JNG.VOL 1/2020** **Tarehe..............**

Ndugu.........................................
Mzazi/Mlezi wa ...............................
S.L.P.........
....................

**YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NATTA MWAKA 2021.**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao ....................................................... amechaguliwa kujiunga na Kidato cha **I** mwaka **2021** katika shule hii ambapo atapata Elimu na hatimaye kulitumikia Taifa. KamaMzazi/Mlezi unapaswa kumuasa mwanao azingatie masomo pamoja na taratibu zote za shule na kumpa mahitaji yote ya shule ili aweze kufanikisha azma hii.

Shule ya Sekondari Natta iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara, umbali wa Kilomita 40 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya-Mugumu.

Shule itafunguliwa Muhula wa kwanza tarehe **11/01/2021.** Muda wa kuripoti ni kuanzia **saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 mchana siku za kazi tu**. Mwanafunzi anatakiwa kuwa ameripoti shuleni si zaidi ya wiki mbili tangu shule kufunguliwa. Mara mwanafunzi afikapo shuleni **aripoti Ofisini kwa Makamu Mkuu wa Shule kwa mapokezi na usajili.** Makamu Mkuu wa shule atahakikisha kwamba mwanafunzi amekuja na sare pamoja na vifaa vingine kama vilivyoagizwa kwenye fomu ya kujiunga na Shule.

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;

i. **Kiti na dawati kwa ajili ya kusomea (Aje navyo)**
ii. Fomu iliyojazwa na Daktari kuhusu Afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form).
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal Particularas Form).
iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.
v. **Aje na Ream moja ya karatasi (Double A)**
vi. **PICHA (PASSPORT SIZE) moja angalau kwa Mzazi/Mlezi atakayeandikishwa kwenye FOMU iliyopo kwenye ukurasa wa NNE (04).**

Pamoja na barua hii naambatanisha orodha kamili ya vifaa vya lazima mwanafunzi anavyopaswa kuja navyo na fomu mbili anazotakiwa kujaza na kuja nazo wakati wa kuripoti shuleni.

**ZINGATIA: HATUPOKEI MWANAFUNZI SIKU NA SAA AMBAZO SIYO ZA KAZI.**

HEADMASTER
NATTA SEC. SCHOOL
MUGUMU

...............................
MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**
**SHULE YA SEKONDARI YA NATTA**

**ORODHA KAMILI YA MAHITAJI YA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI**

**SARE YA SHULE.**

**I. WAVULANA**

- Mashati mawili meupe mikono mifupi.
- Suruali mbili rangi ya **Damu ya Mzee** zenye mifuko miwili ya pembeni na mmoja nyuma kulia **zisizobana na zisiwe "MODO"**
- T-SHIRT moja ya rangi ya KIJANI zenye kola isiyo na maandishi yoyote. Huvaliwa siku ya Ijumaa na siku za KAZI shuleni.
- Sweta la rangi ya Damu ya Mzee lenye mshono au shingo ya **"V".**
- Soksi jozi 2 za rangi nyeusi.
- Tai ya rangi ya damu ya Mzee.
- Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu.
- Aje na viatu na nguo za michezo (Track Suit) ya rangi ya "Light Blue" kwa Kidato cha Kwanza Pamoja na raba.
- Mkanda wa ngozi rangi nyeusi wa ukubwa wa kati usio na "bicross" kubwa.

**II. WASICHANA**

- Mashati mawili meupe mikono mifupi.
- Sketi mbili ndefu zinazofika katika kifundo cha mguu kwenye kisigino rangi ya **Damu ya Mzee MSHONO WA RINDA BOX**
- T-SHIRT moja ya rangi ya KIJANI zenye kola isiyo na maandishi yoyote. Huvaliwa siku ya Ijumaa na siku za KAZI shuleni.
- Sweta la rangi ya Damu ya Mzee lenye mshono au shingo ya **"V".**
- Soksi jozi 2 za rangi nyeupe.
- Tai ya rangi ya damu ya Mzee.
- Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu.
- Mnunulie viatu na nguo za michezo (Track Suit) ya rangi ya "Light Blue" kwa Kidato cha Kwanza Pamoja na raba.

**N.B: Suruali na sketi zitapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 19,000/= kwa sketi moja na Tsh. 18,000/= kwa suruali moja.**

KUMBUKA: **Mwanafunzi wa shule hii hapaswi kuja na nguo nyingine yoyote tofauti na hizo hapo juu. Nguo za nyumbani hazitakiwi kabisa shuleni hapa.**

**VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI**

1. Mathematical set
2. Kamusi (English Dictionary)
3. Madaftari makubwa (Counter Books) yasiyopungua 10.
4. Kalam na penseli
5. Ream moja (Double A) kwa ajili ya mitihani, mazoezi na majaribio
6. Aje na vitabu vya masomo angalau matatu ili kupunguza uhaba wa vitabu shuleni **(ni mali ya mwanafunzi)**
7. Begi la mgongoni la kubebea daftari na vifaa vya kusomea.

**VIFAA VYA USAFI**

1. Ufagio aina ya CHELEWA Pamoja na FYEKEO moja (**Kila mwanafunzi**)
2. Ndoo ndogo ya lita 10 (**Wasichana Tu**)
3. Jembe Moja na mpini wake (**Wavulana Tu**)

**HUDUMA YA AFYA NA MATIBABU**

Huduma ya afya na matibabu ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi. Hata hivyo uongozi wa shule unashauri mwanafunzi akatiwe kadi ya **BIMA YA AFYA YA NHIF** kwa **Tsh. 50,400/=** ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wakati na kupunguza gharama.



HEADMASTER

## SHERIA ZA SHULE

Shule ya Sekondari Natta inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

### A. KILA MWANAFUNZI WA SHULE HII NI LAZIMA AZINGATIE MAMBO YAFUATAYO;

a) Heshima kwa viongozi wazazi wafanyakazi wote na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Kuhudhuria katika kila shughuli ndani na nje ya shule pale unapohitajika.
**c) Kusaini mkataba maalum wa taaluma shuleni kuhusu kufanya vizuri na kufaulu mitihani.**
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuepuka kuwa nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
e) Kutunza usafi na mazigira ya shule wakati wote.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote mwanafunzi anapokuwa ndani ya shule na anapotakiwa shuleni.
g) Kufuata ratiba ya shule wakati wote, kusoma kwa bidii na kufanya kazi za darasani bila kutegea.
h) Kujisomea kabla ya kulala anapokuwa nyumbani (mzazi/mlezi amsimamie mwanaye).

**ONYO: NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI YEYOTE KUJA SHULENI AKIWA AMEVAA NGUO ZA NYUMBANI (ISIPOKUWA KWA MAELEKEZO MAALUM).**

### B. MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA

a) Kuvuta sigara.
b) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na ndevu, kusuka na kunyoa kihuni (Mitindo isiyofaa).
c) Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule ndani ya eneo la shule.
d) Kupigana/ kuchochea ugomvi au kumpiga mtu yeyote.
e) Kuiga mitindo ya kihuni isiyofaa katika jamii.
f) Kwenda nje ya shule bila ruhusa kutoka kwa mwalimu.
**g) Mwanafunzi kumiliki au kutumia au kukutwa na simu au "Line" sehemu yoyote katika mazingira ya Shule.**
h) Kupeleka mgeni sehemu nyingine isiyohusika tofauti na maeneo yaliyoelekezwa.
i) Kwenda kwenye nyumba za walimu ama watumishi wasio walimu bila ruhusa au sababu ya muhimu.
j) Kuingia au kutembelea maeneo ya kuuzia vileo na majumba ya starehe.

### C. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:

1. Wizi.
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga.
3. Uvutaji bangi.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya/ Miadarati.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. **Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.**
8. Kudharau Bendera na Wimbo wa Taifa.
9. Kuoa/Kuolewa.
10. Kusababisha mimba.
11. Kusaidia kutoa mimba.
12. Kugoma, Kuchochea na kuongoza fujo zenye kuvuruga amani, usalama wa watu na mali ya umma.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kutoingia katika vipindi/ darasani au kukataa kufanya mtihani na mazoezi.
15. Kudharau/ kutowaheshimu/ kuwagomea viranja wa shule.
16. **Mwanafunzi kumiliki au kutumia au kukutwa na simu au "line" katika mazingira ya Shule.**

**ZINGATIA:**

1. **MWANAFUNZI AKIKUTWA NA SIMU SHULENI AU LINE ATALIPA GHARAMA ZA UHARIBIFU WA MIUNDO MBINU NA ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA HAKUTAKUWEPO MJADALA.**
2. **MWANAFUNZI AKIHARIBU MALI YA SHULE AU MIUNDO MBINU PAMOJA NA KUFUKUZWA SHULE NI LAZIMA ATALIPA GHARAMA ZA UHARIBIFU ALIO UFANYA!**

MKUU WA SHULE

 HEADMASTER

**OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**
**SHULE YA SEKONDARI NATTA**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

1. Jina kamili (Kama ilivyo kwenye TSM 9) ……………………………………………………………
2. Anwani ya nyumbani ……………………………………………………………………………..
3. Tarehe ya kuzaliwa …………………
4. Mahali ulipozaliwa, Kijiji/Mtaa…………………………
   Kata…………………………Tarafa…………….. Wilaya……………………………………..
   Mkoa………………………………………
5. Mahali unapoishi kwa sasa Kijiji/Mtaa…………………..
   Kata………………………Tarafa……………… Wilaya…………………………………..
   Mkoa………………………………………
6. Shule ya Msingi ulikotoka……………………………………………………………………
   Anwani…………………………………………………………………………………………
7. Dini/Dhehebu………………………………………………………………..
8. Kabila……………………………………………………………………………
9. Taifa (Mtanzania/Si Mtanzania………………………………………………..

**10. JAMAA KATIKA FAMILIA AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA TAARIFA ZAKO MUHIMU KWA MASUALA YAHUSUYO SHULE:**
**(JAZA SEHEMU ZOTE NNE, PAMOJA NA ANGALAU PASSPORT SIZE ZA MZAZI/MLEZI)**

i) **Jina la Baba**……………………………………………… Namba ya Simu …………………………
   Anaishi/ Haishi……………………………………
   Kazi yake……………………………………………………..
   Anwani…………………………………………… PICHA

ii) **Jina la Mama**…………………………………………… Namba ya Simu ……………………..
   Anaishi/ Haishi……………………………………
   Kazi yake………………………………………………………………
   Anwani………………………………………………………… PICHA

iii) **Jina la Mlezi (1)**…………………………Uhusiano……………Namba ya Simu ………………
   Kazi yake…………………………………………………………
   Anwani………………………………………………………………………… PICHA

iv) **Jina la Mlezi (2)**………………………… Uhusiano……………Namba ya Simu ………………
   Kazi yake ……………………………………………………………………
   Anwani……………………………………………………………………….. PICHA

Mimi (Mwanafunzi)……………………………………………………… nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli. Ahadi yangu, Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii na ninahaidi kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.

………………………………………  ……………………..
Sahihi ya Mwanafunzi  Tarehe

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi)……………………………………………………….. ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………… nimeyasoma masharti na sheria za shule ya Sekondari Natta ambako kijana/binti yangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa Shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

………………………………………  ……………………
Sahihi ya Mzazi/Mlezi  Tarehe

**NATTA SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Natta Secondary school,
P.O.Box 192,
**MUGUMU-SERENGETI.**

Date…………………

To Medical Officer,
………………………………………
………………………………………
………………………………………
Ref.…………………………………………………………………………
(NAME OF STUDENT)

Please examine the above-named Student as per Medical examination form below,

………………………………………
**HEADMASTER**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**
(To be completed by Government Medical Officer)
Full Name………………………………………………………………………………………………..
Age………………Height……………..(cm)Weight……………………………..(Kg)

1. Blood count (Red and White)……………………………………………………………………
2. Stool Examination………………………………………………………………………………..
3. Urinary analysis……………………………………………………………………………………
4. STDs and other V.D………………………………………………………………………………
5. T.B and Leprosy test………………………………………………………………………………..
6. Eye test……………………………………………………………………………………………
7. Ear test……………………………………………………………………………………………
8. Chest ……………………………………………………………………………………………
9. Abdominal test…………………………………………………………………………
10. Blood Group **(Very Crucial)**……………………………………………………………………………
11. Spleen……………………………………………………………………………………………

Any additional defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g Sickle cell),
…………………………………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

I have examined the above-named student and I certify that he/she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.

Signature…………………………………………Date……………………

Station……………………………………………………………………………

Designation and Official Stamp………………………………………………

**THANK YOU**